# Connect for Success (jiunge na ufanisi)

## Ripoti ya Ziara ya Kituo: Shule ya Msingi ya College View

COLORADO
Department of Education

## Utangulizi

Shule ya Msingi ya College View, shule ya Misaada katika Denver Public Schools, inahudumia takriban wanafunzi 300 wa Chekechea (ECE) – darasa la 5. Mnamo tarehe 9 Mei, 2023, Timu ya Ukusanyaji Data (DCT) yenye wanatimu kutoka Idara mbalimbali kutoka Idara ya Elimu ya Colorado (CDE) ilitembelea College View ili kupata ufahamu wa kina na kujua msingi wa shughuli zinazofanywa shuleni.

Kabla ya ziara ya CDE, wafanyakazi wa College View, wazazi, na wanafunzi walialikwa kushiriki bila kujitambulisha katika utafiti kuhusu mbinu na taratibu za sasa. CDE ilipokea na kuchambua majibu kutoka kwa wazazi 22 na wafanyakazi 31: Walimu 14 (asilimia 45) na 17 (asilimia 55) ya wafanyakazi wa kuwasaidia walimu kufunza, viongozi na wafanyakazi wa usaidizi. Kwa jumla, wanafunzi 105 walishiriki katika utafiti huo, ikiwakilisha hasa wanafunzi wa darasa la 3 - 5. Pia, DCT ilifanya mahojiano tisa na vikao saba vya kupokea maoni na wasimamizi, walimu, wafanyakazi wanaotoa huduma maalum, wafanyakazi wa usaidizi, na makundi ya wanafunzi na ziara tano za uchunguzi wa darasani.

### *Nguvu za Shule Zitakazochangia katika Utekelezaji wa Mikakati ya HAS kwa Mafanikio*

- Wafanyakazi wanahisi vizuri na kuungwa mkono.
- Wanafunzi wanahisi kukubalika na kuthaminiwa jinsi walivyo.
- Uongozi umetoa fursa kwa wafanyakazi kuchukua majukumu ya uongozi.
- Timu za kiwango cha darasa hukutana mara kwa mara na makundi ya kiwango cha darasa.
- “What I Need Time” (WIN)/“Wakati wa Kitu Ninachohitaji” umebuniwa kwa ajili ya wanafunzi kupokea usaidizi unaowalenga.
- Shule imeshirikiana na baadhi ya washirika wakuu wa nje.

Data iliyokusanywa wakati wa ziara ya shule zilitumiwa kutambua uwezo wa College View na fursa za kutumia masomo tuliyojifunza kutoka kwa utafiti wa Shule za Wanafunzi wenye Matokeo Bora za Colorado (HAS) (http://www.cde.state.co.us/fedprograms/dper/evalrpts#has). Matokeo hayo yamelingana na Vikoa Vinne vya West Ed vya Mfumo wa Uboreshaji wa Haraka wa Shule, ambao unajumuisha (1) Uongozi kwa ajili ya Uboreshaji wa Haraka, (2) Usimamizi wa Vipaji, (3) Mabadiliko ya Mafunzo, na (4) Mabadiliko ya Utamaduni na hali iliyopo. CDE imepitisha na kurekebisha Vikoa Vinne vya WestEd vya Uboreshaji wa Haraka wa Shule ili kuunda Mfumo wa Uboreshaji wa Haraka wa Shule wa Colorado (https://www.cde.state.co.us/fourdomains). Mapendekezo (yaliyoonyeshwa kwa fonti ***nzito ya mlalo***) yaliyobainishwa katika ripoti hii yanatokana na mikakati na mbinu zilizotekelezwa na HAS ambazo zinalingana na uwezo wa College View na sehemu zinazohitaji uboreshaji zilizobainishwa na DCT.

Timu kutoka kwa College View itazuru mojawapo ya Shule za Wanafunzi wenye Matokeo Bora ili kupata maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wake wa mikakati iliyoangaziwa katika utafiti wa Shule za Wanafunzi wenye Matokeo Bora na kubainisha zile zinazolingana vyema na zinazofaa kwa mahitaji ya College View. Mapendekezo yafuatayo, pamoja na mafunzo tuliyojifunza kutokana na utafiti wa HAS, ziara kwa mojawapo ya shule za HAS, na tathmini ya mahitaji inayohusiana na mpango wa shule nzima ya shule ya Misaada ya College View na/au Mpango wa Pamoja wa Uboreshaji (UIP) unapaswa kutumika kuandaa mpango wa utekelezaji wa ruzuku ya Connect for Success (CFS). Mojawapo ya nguvu zilizobainishwa katika HAS ni kwamba kila shule inaipa vipaumbele mipango miwili hadi mitatu muhimu kwa mwaka. ***Kwa hivyo, inapendekezwa kuwa College View ichague pendekezo moja au mawili katika ripoti hii ambayo yanalingana vyema na dhamira yake, maono, na vipaumbele vya sasa ili kubuni mpango wa utekelezaji wa CFS. Kwa kupunguza vipaumbele, College View itaweza kuhakikisha utekelezaji thabiti na wenye nguvu wa mipango iliyochaguliwa.***

### Mapendekezo

- Kupanua na kulinda muda ili kujenga mahusiano kati ya wafanyakazi wote katika ngazi zote.
- Kubuni upya dhamira, maono na malengo ya College View, huku wadau wote wakihusika pakubwa katika harakati hizo.
- Kujenga juu ya mifumo ya sasa ili kuhakikisha uwezo wa wafanyakazi kudumisha matarajio ya juu ya mafunzo.
- Kupanua michakato ya sasa ili kudumisha matarajio ya juu ya tabia kwa wanafunzi wote.
- Kujumuisha wataalamu na wafanyakazi wengine wa usaidizi wa mafunzo katika fursa za kitaaluma za kujifunza, ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mikakati ya kitabia na mafunzo.

## Nguvu za Shule na Fursa za Kutekeleza Mikakati Tuliyojifunza kutoka kwa HAS

### *Mahusiano Yanathaminiwa*

Umuhimu na thamani ambayo College View inaweka kwa mahusiano, jumuiya, ushirikiano, na kufanya kazi kwa pamoja iliangaziwa kama njia bora ya kupata mafanikio yake. Wafanyakazi wanathamini viongozi imara wa College View na falsafa yao ya kuruhusu kila mfanyakazi kuuliza maswali na kutoa maoni yao kuhusu mambo tofauti. Wafanyakazi wanahisi kuonekana, kuthaminiwa, na kupongezwa, na kwamba wanaweza kufanya kazi jinsi walivyo na kusherehekewa kwa jinsi walivyo. Wazazi walijadili hali ya ukaribishaji wa College View, pamoja na mipango mbalimbali kama vile soko la wakulima, tamasha, hafla ya kunywa kahawa na mwalimu mkuu, na hafla za kitamaduni. Utafiti na mahojiano ya wanafunzi yalibainisha uhusiano wao thabiti na walimu na wafanyakazi. Idadi kubwa ya wanafunzi 132 waliohojiwa (asilimia 94) wanahisi kuwa watu wazima shuleni wanawajali.

Ingawa wafanyakazi kwa ujumla wanathamini na kupongeza hisia nzito ya ushirikiano na jumuiya, hasa kati ya timu na vikundi vya kiwango moja cha darasa, wangefurahia fursa zaidi za kushirikiana kiwima, katika taaluma na majukumu. Wanne kwa watano (asilimia 80) ya wafanyakazi 30 wanakubali kuwa ushirikiano na upangaji wa pamoja hutokea mara kwa mara kati ya walimu wa elimu ya jumla katika madarasa yote. Wafanyakazi wa College View wamefurahishwa na idadi kubwa ya wafanyakazi wanaorejea katika mwaka wa 2023-24 na fursa za kuendelea kujenga mahusiano. Hasa, walimu wageni na walimu wapya shuleni wanatarajia kunufaika kutokana na fursa zaidi za kimakusudi za kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wafanyakazi wa muda mrefu wa College View.

HAS inathamini na kuipa kipaumbele mahusiano kati ya viongozi wa shule, walimu, wataalamu, wafanyakazi wengine, familia na wanafunzi. Wakati na juhudi zimewekwa katika kujenga na kudumisha mahusiano thabiti kwa kufahamiana katika kiwango cha kibinafsi kinachojumuisha asili ya kitamaduni. Viongozi wa HAS huhakikisha kuwa wafanyakazi wote (walimu wapya, wataalamu wanaosaidia katika mafunzo, n.k.) wana fursa za kuangalia na kujifunza kutoka kwa mifano thabiti ya kuigwa na kupata usaidizi wanaouhitaji ili kufaulu katika majukumu yao. HAS imetumia muda pia kukuza mahusiano, kuunganisha timu zilizoko ili kukuza hisia ya kukubalika katika shule yote. ***DCT inapendekeza College View iendelee kutilia mkazo katika kukuza mahusiano thabiti. Iendelee kukuza uwezo wa wafanyakazi na kuruhusu ziara za darasani ili kuonyesha sehemu za utaalamu na kukuza mahusiano yanayoaminika katika shule yote.***

### *Kutumia Lugha Moja kwa ajili ya Utoaji wa Ujumbe Thabiti Kuhusiana na Maono ya Shule Yote na Malengo Yanayopewa Kipaumbele*

Wafanyakazi wa College View wanaonyesha wazi dhamira ya pamoja kwa wanafunzi na familia zao. Idadi kubwa (asilimia 95) ya wazazi 22 waliohojiwa wanakubali kuwa mafunzo yamepewa kipaumbele katika College View. Mahojiano ya wafanyakazi na vikao vya kupokea maoni vilionyesha dhamira ya pamoja ya kushughulikia mahitaji ya kujifunza ya wanafunzi wote kwa ufanisi. Vile vile, asilimia 94 ya wafanyakazi 31 wanakubali kuwa wafanyakazi "wengi" au "wote/asilimia kubwa" wana hisia ya kuwajibika na kujitolea kuboresha ufaulu wa wanafunzi wote, na asilimia 97 wanakubali kuwa wafanyakazi "wengi" au "wote/asilimia kubwa" wana matarajio makubwa kwa wanafunzi.

DCT ilisikia kuhusu malengo yaliyo wazi ya kitaaluma na utafutaji wa kimakusudi wa rasilimali (yaani, ruzuku, ubia) ili kutimiza malengo hayo kutoka kwa uongozi. Hata hivyo, uchunguzi na mahojiano yanaonyesha haja ya kufafanua na kuimarisha matarajio ya wafanyakazi kuhusu kutekeleza ruzuku nyingi na mipango mingine ya shule na wilaya. Matarajio tofauti yamezua mkanganyiko kuhusu cha kufanya na jinsi ya kutekeleza. Robo tatu tu (asilimia 77) ya wafanyakazi 26 wanakubali kuwa walimu "wengi" au "wote/asilimia kubwa" hutumia rubriki za kawaida, mifano na orodha za ukaguzi. Ingawa asilimia 87 ya wafanyakazi 30 waliohojiwa wanasema kuwa viongozi wa shule wanahakikisha kuwa wafanyakazi wote wanajumuishwa katika kufanya maamuzi, DCT ilisikia kuwa wafanyakazi wanahitaji kujumuishwa kwa uwazi zaidi katika kufanya maamuzi ili kuhakikisha uthabiti wa matarajio ya ujumbe katika mipango mbalimbali. Hii ni pamoja na ujumbe unaohusiana na jinsi ruzuku na ubia unavyosaidia juhudi za pamoja kuelekea kufikia vipaumbele vilivyokubaliwa.

Utekelezaji wenye mafanikio unategemea ufuatiliaji wa mara kwa mara na kupokea maoni kuhusu matarajio na zana za kawaida ili kuhakikisha utekelezaji thabiti. Kuhusu mara ambazo wasimamizi hutembelea madarasa yote ili kufuatilia utekelezaji mzuri wa mipango ya mafunzo, nusu (asilimia 52) ya wafanyakazi 31 wanasema "kila wiki," robo (asilimia 26) wanasema "kila mwezi," asilimia 19 wanasema "mara 3-5 kwa mwaka," na asilimia tatu wanasema "mara 1-2 kwa mwaka." Pia, asilimia 87 ya wafanyakazi 31 wanakubali kwamba mafunzo ya kitaaluma huchaguliwa, kufuatiliwa, na kutathminiwa "kila wakati" (17, asilimia 55) au "kwa kawaida" (10, asilimia 32) ili kuhakikisha kuwa yanaunga mkono malengo yaliyotambuliwa na kuboresha ufanisi wa walimu; wachache wanasema "wakati fulani" (3) au "mara chache" (1).

HAS imebuni maono na matarajio yaliyo wazi, na mara kwa mara huyawasilisha kwa wadau wote (wanafunzi, familia, walimu, wafanyakazi, na viongozi wa shule) kwa uwazi. ***Huku wafanyakazi wengi wakirejea mwaka ujao, College View ina fursa nzuri ya kuendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi, kufafanua wajibu na majukumu, na kufuatilia kwa uwazi utekelezaji wa malengo yanayopewa kipaumbele. DCT inapendekeza viongozi wa College View kushirikiana na wafanyakazi wote ili kubuni upya na kuwasiliana vipaumbele na malengo ya kawaida, kisha kubuni mpango wa kuhakikisha utekelezaji bora. Ufafanuzi huu utakuwa wa maana sana kwani uongozi unahakikisha kuwa ruzuku na ubia haziko katika ushindani, lakini zinasaidia mahitaji na malengo ya shule kwa uwazi.***

## *Kujenga juu ya Mifumo ya Sasa ili Kuhakikisha Matarajio ya Juu ya Mafunzo kwa Wanafunzi Wote*

College View imetenga wakati na rasilimali muhimu katika kutekeleza mpango wa mafunzo ulioboreshwa. DCT ilibainisha kuwa sehemu za mafunzo zilitengenezwa kimakusudi, zikiwa na nyenzo muhimu za elimu zilizowekwa na zinazopatikana kwa urahisi. Kwa ujumla, maoni ya walimu hayakuwa ya kukosoa, na wafanyakazi wanaonekana kuwa na maelewano mazuri na wanafunzi. Uchunguzi wa darasa la DCT ulionyesha mafunzo ya moja kwa moja na matumizi ya lugha ya kufunza inayozingatia mada. Mahojiano ya wafanyakazi yalionyesha mafanikio kadhaa ya mafunzo, hasa utekelezaji wa Ruzuku ya Kusoma na Kuandika ya Wanafunzi wa Chekechea (ELG) na usaidizi wa wakufunzi wa kitaaluma katika kuhakikisha kuwa mahitaji ya wanafunzi yanatambuliwa na kutimizwa.

Ingawa wafanyakazi wanajivunia na kufurahishwa na ukuaji huu wa mafunzo, kulikuwa na makubaliano kwamba baadhi ya sehemu zinahitaji kuzingatiwa zaidi. Wengi wa wafanyakazi 30 wanakubali kuwa walimu "wengi" au "wote/asilimia kubwa" hutumia mikakati mbalimbali ya kufunza ili kushughulikia mahitaji ya kila mwanafunzi (asilimia 90) na walimu wanawajibika katika ufaulu wa wanafunzi wote na mafunzo yanayotolewa yanahakikisha kuwa wanafunzi wanapata umilisi wa stadi wanazofunzwa (wote 83%). Hata hivyo, robo tatu tu ya wanafunzi 103 wanakubali kuwa walimu huwahimiza mara kwa mara kutia bidii katika kazi yao (asilimia 78) au kuhakikisha kuwa vipindi vya kujifunza na vya darasani vinavutia (asilimia 75). Asilimia 39 pekee ya wanafunzi wanaripoti kuwa wanafahamishwa kuhusu matokeo yao kwenye majaribio au tathmini nyinginezo mara kwa mara. Katika kuzingatia wanafunzi walio na mahitaji ya ziada, nusu (asilimia 58) tu ya wafanyakazi 31 wanahisi kuwa mafunzo kwa wanafunzi wenye ulemavu katika madarasa ya elimu ya kawaida ni "mazuri" au "bora." Kulingana na mahojiano na uchunguzi, DCT haina uhakika ikiwa College View inawatayarisha vya kutosha wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kiwango chao kinachofuata cha elimu kwa mafunzo yaliyo wazi yatakayowezesha ufasaha wa Kiingereza.

Ingawa mahojiano ya wafanyakazi yaliangazia kiwango cha ushirikiano, kama ilivyotajwa hapo juu, wafanyakazi walionyesha kutaka fursa za ziada za kuimarisha uhusiano na kuendelea kujenga uaminifu, na kuimarisha utekelezaji thabiti wa mikakati ambayo huathiri vyema wanafunzi katika viwango vyote vya darasa na sehemu za maudhui. Kando na data katika sehemu ya *Mahusiano Yanathaminiwa* hapo juu, asilimia 72 ya wahojiwa 29 waliripoti kuwa walimu wanapewa muda wa kutosha kupanga vitengo/masomo pamoja na walimu wenzao wa kiwango moja cha darasa au maudhui.

Mbinu za HAS ni pamoja na kuwa na kutumia lugha na mbinu za pamoja za kufunza. HAS imelinganisha mbinu katika sehemu zote za maudhui na viwango vya darasa ili kuongeza ufanisi na ufaafu wa muda wa darasani na wa mafunzo. ***DCT inapendekeza kuwa wafanyakazi wa College View wafikie makubaliano ya shule nzima kuhusu mbinu za kufunza na lugha ya kutekelezwa. Kutoa muda wa kutosha kwa wafanyakazi kushirikiana na timu za kiwango moja cha darasa, kiwima na wataalamu, ili kuhakikisha kuwa mafunzo ni thabiti, yanashirikisha, yanafaa, yanatoa changamoto, na yanatimiza mahitaji ya wanafunzi. Uchunguzi wa mara kwa mara wa darasani na kuyatembelea madarasa kutasaidia kuhakikisha utekelezaji thabiti na kusaidia katika kubuni hatua zinazofuata.***

## *Kushikilia Matarajio ya Juu ya Tabia Kila Wakati*

Mahojiano, vikao vya kupokea maoni, na uchunguzi ulifahamisha DCT kuwa kuna mifumo kadhaa ya kusaidia tabia ya wanafunzi na afya ya akili. Wafanyakazi kadhaa walisema kuwa "HUB" ni chombo na nyenzo muhimu ya kupata maelezo muhimu ya shule, ikiwa ni pamoja na fomu ya rufaa ya tabia. Wafanyakazi walitaja pia kuwa kuna usaidizi kwa walimu wakati wa matukio ya tabia isiyopendeza ya wanafunzi. Wafanyakazi walijadili kuwa mifumo iliyoanzishwa ya kushughulikia tabia haifuatwi mara kwa mara.
Sababu za kutotekelezwa mara kwa mara si wazi, lakini baadhi wanapendekeza kuwa kunatokana na kina cha uzoefu wa kufunza, kutofahamu nyenzo, na tofauti za kiitikadi. Robo tatu pekee (asilimia 74) ya wafanyakazi 31 wanakubali kuwa wafanyakazi "wengi" au "wote/asilimia kubwa" wanasisitiza matarajio ya tabia ya wanafunzi kwa uwazi na mara kwa mara. Mahojiano pia yalionyesha ukosefu wa matokeo wazi kwa wanafunzi, jambo ambalo huwasilisha jumbe mseto na kuwakatisha tamaa wafanyakazi. Wanafunzi walitafakari pia jinsi tabia inavyoathiri jumuiya; kati ya wanafunzi 74 waliohojiwa (31 hawakujibu), thuluthi mbili (asilimia 68) wanahisi salama kimwili shuleni "mara nyingi" au "kila wakati," na nusu (asilimia 52) ya wanafunzi 103 wanahisi salama kihisia shuleni "mara nyingi" au "kila wakati."

Matarajio ya tabia yanaonyeshwa kwa uwazi kote katika HAS na walimu wote wanafuata kanuni/sheria na matokeo sawa ya kitabia. Walimu wa HAS walieleza kuwa katika madarasa ya kwanza, wiki kadhaa za kwanza za kila mwaka wa shule zimetengwa kwa ajili ya kubuni ratiba za darasani na kuangazia matarajio. Kwa sababu wapo katika madarasa yote, wanafunzi wanaorejea tayari wanafahamu taratibu na matarajio ya darasani na husaidia kuwafunza wanafunzi wapya. ***DCT inapendekeza kujenga juu ya miundo iliyopo ya tabia na kukagua upya/kufafanua upya taratibu za tabia. Kujumuisha matarajio wazi kwa wanafunzi na majukumu maalum ya wafanyakazi ya kushughulikia tabia ya wanafunzi. Kupitia uundaji na utekelezaji thabiti wa taratibu za tabia katika mwaka wote wa shule, walimu watajua jinsi ya kushughulikia, mtu wa kuwasiliana naye, na jinsi ya kutekeleza matokeo yaliyokubaliwa. Pia, wanafunzi watatambua matarajio ya tabia na kushikiliwa kwa matarajio hiyo ya juu katika kila sehemu wanayotembelea.***

## *Kuimarisha Matumizi ya Wafanyakazi wa Kusaidia Katika Mafunzo*

DCT ilifahamishwa kuwa College View imeanzisha na inathamini mtindo wa "kuza mmoja wenu", ambapo wafanyakazi kadhaa hushiriki. Mtazamo huu, wa kuheshimu kila mchangiaji kama sehemu muhimu ya elimu ya wanafunzi wote, ni nguvu. Pia, wataalamu wanaowasaidiwa walimu wanatamani kukuza ujuzi wao katika kutoa hatua za uingiliaji kati za elimu na usimamizi wa tabia. Hii ilitajwa zaidi ya mara moja katika mahojiano mbalimbali. Haionekani kuwa wafanyakazi wa kusaidia katika mafunzo wanaweza kufikia fursa za maendeleo ya kitaaluma na uangalizi kama walimu, ingawa ushirikiano unaonekana kutokea wakati mwingine. Kulingana na data ya uchunguzi, kati ya wafanyakazi 29 (2 "hawajui"), asilimia 83 wanahisi kuwa ushirikiano na mipango ya pamoja kati ya walimu na wafanyakazi wa kusaidia katika mafunzo hutokea mara kwa mara. Kati ya wafanyakazi 30 (1 "hakujua"), asilimia 73

wanakubali kuwa mafunzo ya wanafunzi wenye ulemavu katika mipango ya uingiliaji kati au ya kuwaondoa darasani ni “nzuri” au “bora.” Haikuwa wazi ni kiasi gani cha uingiliaji kati wa mafunzo ya kuondolewa darasani na usimamizi wa tabia hutolewa na wafanyakazi wanaowasaidia walimu. Kwa kuwa wafanyakazi wa usaidizi hutumia muda wao mwingi na wanafunzi, ni muhimu kuhakikisha kuwa wamewezeshwa kikamilifu ili kutoa hatua za kitaaluma za uingiliaji kati na usaidizi unaofaa wa kitabia. Lugha ya kawaida na mikakati ya uingiliaji kati ni muhimu kama sehemu ya stadi zao kama ilivyo kwa walimu.

HAS inaweka mikakati maalum kwa ajili ya uajiri, uhifadhi, na mafunzo ya wafanyakazi wanaowasaidia walimu. Wataalamu wa kuwasaidia walimu hufanya kazi mara kwa mara na walimu wakuu wa shule na viongozi wa walimu ili kujenga uwezo, na kazi zao zinafuatiliwa mwaka mzima.
Wanapewa mafunzo kuhusu hatua za uingiliaji kati wanazotekeleza, mara nyingi hupokea mafunzo sawa na walimu na mafunzo ya ziada kama inavyohitajika. Wanathaminiwa kama washiriki wataalamu wa timu, wanaochangia kwa usawa katika dhamira ya shule. ***Inapendekezwa kuwa College View iwekeze katika kuajiri, kuhifadhi, mafunzo, ufuatiliaji, na kuwafundisha wafanyakazi wanaowasaidia walimu ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata elimu ya kina na utekelezaji thabiti wa mikakati ya kitabia na mafunzo.***

## Hatua Zinazofuata

Katika kipindi cha ruzuku ya CFS, College View itapata fursa kadhaa za kujadiliana na HAS ili kupata maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wao wa mikakati iliyoangaziwa katika utafiti wa HAS na kutambua mbinu ambazo zinalingana vyema na zinafaa kwa mahitaji ya College View. Kwa kutumia matokeo ya Tathmini yake ya Kina ya Mahitaji (CNA), mapendekezo kutoka kwa ripoti hii, na mafunzo tuliyojifunza kutokana na majadiliano na HAS katika vikao vya kila mwezi vinavyopangwa na CDE, College View lazima itambue kipaumbele kimoja au viwili, kubuni malengo, na kuwasilisha mpango wa utekelezaji wa Ruzuku ya CFS, ambao unapaswa kutumika kuimarisha Mpango wake wa Shule Nzima ya Shule ya Wanafunzi wenye Mapato Duni na/au UIP. Inatarajiwa kuwa nakala ya ripoti hii/muhtasari wa mapendekezo itashirikiwa na wafanyakazi wa shule, wanachama wa bodi ya shule, washirika wa wilaya, Mkufunzi wa Utekelezaji wa CFS, na familia/wazazi ili kupata usaidizi wa kubuni mpango wa utekelezaji.

**Timu ya Ukusanyaji Data na Waandishi wa Ripoti**

- **Christina Adeboye Sullivan**
- **Rachel Echsner**
- **Patty Gleason**
- **Laura Meushaw**
- **Wendy Sawtell**
- **Rachel Temple**